



Kilimanjaro Mountain Resort Ltd.

Cool Relaxation & Country Adventure, all Seasons

Kyalla - Marangu West

P.O.Box 301

Marangu

TANZANIA

EAST AFRICA

Tel: +255 (0) 27 2758950

Mobile: +255 (0) 754 693461

+255 (0) 754 999 755

Fax: +255 (0) 27 275 8949

Email: kiliresort@iwayafrica.com

www.kilimanjaromt resort.com

REF : kmr/04/2020

01/04/2020

Meneja

TRA Moshi.

Ndugu,

**YAH: TAARIFA YA KUFUNGA HOTELI YA KILIMANJARO MOUNTAIN RESORT
MARANGU KWA MIEZI MITATU KUENZIA TAREHE 01/04/2020 – 30/06/2020.**

Tafadhali rejea kichwa cha habari kilichoandikwa hapo juu.

Kufuatia upungufu mkubwa wa watalii wa kutoka nchi za Marekani na Ulaya na pia adha ya kusambaa kwa ugonjwa wa virusi vya Korona kwenye nchi mbalimbali duniani, Tanzania ikiwa moja wapo, tunapenda kutoa taarifa kuwa hoteli yetu imesitisha kabisa kutoa huduma kwa muda wa miezi mitatu kama ilivyoandikwa hapo juu.

Ni tegemeo letu kuwa ugonjwa huu utapita na kutuacha salama na kurejesha hali ya biashara ya utalii kama ilivyokuwa hapo awali.



Wako katika ujenzi wa taifa
Kilimanjaro Mountain Resort

.....
Eng. Mark William Njiu.
Mkurugenzi mkuu.

cc: Ndamallya & Co.



Kilimanjaro Mountain Resort Ltd.

Cool Relaxation & Country Adventure, all Seasons

Kyalla - Marangu West

P.O.Box 301

Marangu

TANZANIA

EAST AFRICA

Tel: +255 (0) 27 2758950

Mobile: +255 (0) 754 693461

+255 (0) 754 999 755

Fax: +255 (0) 27 275 8949

Email: kiliresort@iwayafrica.com

[www: kilimanjaromt resort.com](http://www.kilimanjaromt resort.com)

09/08/2020

REF: KMR/088/2020

MENEJA

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

P.O.BOX 1583

MOSHI

Ndugu,

**YAH: TAARIFA YA KUENDELEA KUFUNGA HOTELI YA KILIMANJARO
MOUNTAIN RESORT LTD MARANGU.**

Tafadhali rejea kichwa cha habari kilichoandikwa hapo juu.

Itakumbukwa kuwa hoteli ya Kilimanjaro Mountain Resort ilitoa taarifa ya kufunga hoteli kwa sababu ya tatizo la COVID 19 kupitia barua ya kumb KMR/04/2020 ya tarehe 01/04/2020. Hadi sasa bado hali ya biashara ni mbaya sana hivyo uongozi wa hoteli unatoa taarifa kuwa bado umeendelea kufunga hoteli yake kwa sababu ya upungufu wa watalii kutoka nchi za Ulaya na Marekani. Upungufu huu unatokana na virusi vya korona vilivyozikumba nchi nyingi duniani na kudhoofisha uchumi wao kwa kiasi kikubwa.

Ikizingatiwa kuwa zaidi yaasilimia 98 ya wageni wetu ni watalii wanaokuja kupanda mlima Kilimanjaro, imetuwia vigumu kuendelea na biashara.

Mategemeo yetu ya kufungua hoteli mwezi Julai yalififia baada ya wadau wa utalii (Tour Operators) wakubwa waliokuwa wanatuletea watalii wakiwemo African Walking Company na Peak DMC kuendelea kufuta au kusogeza mbele bookings walizokuwa

wametuletea hivyo kutufanya tukwame kabisa. (Nimeambatanisha nakala za e-mails zao kwa uthibitisho).

Ni tegemeo langu kuwa msimu ujao tutaweza kurudi tena kwenye biashara.



Wako katika ujenzi wa Taifa
Kilimanjaro Mountain Resort.

.....
Eng. Mark Njiu
Mkurugenzi Mkuu

CC. Ndamallya&Co